TANGAZO LA SERIKALI NA. 159 la tarehe 22/2/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 89*

SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA ZA MWAKA, 2019

## SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina na Mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Singida za Mwaka, 2019 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake Afisa yeyote wa halmashauri aliyeidhinishwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Afya" maana yake ni hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii.

"Eneo la wazi "maana yake ni eneo lililo chini ya Halmashauri ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Singida;

"Hati ya usafi" maana yake ni hati itakayotolewa na Afisa

Mwidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi kulingana na Kanuni za Afya.

"Jengo la biashara" maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kufanya biashara iliyokusudiwa.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Taka hatarishi"maana yake ni taka zenye sumu

"Ufugaji wa ndani" maana yake ni ufugaji wa mifugo ndani kwenye chumba maalum katika eneo la mfugaji

"Vyanzo vya maji" maana yake ni maziwa, mabwawa, visima vya aina zote, chemichemi za mito, maji ya mvua.

"Soko'' maana yake eneo lililowekwa na Halmashauri ambalo linatambulika kisheria kufanyia shughuli za biashara.

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

## SEHEMU YA PILI
## USAFI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

4.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi au Mfanyabiashara anayemiliki eneo la nyumba kuhakikisha kwamba anafanya usafi wa mazingira yanayozunguka makazi au eneo lake kwa kuhakikisha kwamba;

(a) majani yanayozunguka nyumba yake yanakatwa au kupaliliwa katika eneo lote hadi mwanzo wa mipaka ya barabara ya mbele ya nyumba yake au eneo lake;

(b) takataka zote zitakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;

(c) mazingira yanayozunguka eneo la nyumba yake yanakuwa safi

wakati wote.

kushiriki shughuli za usafi wa mazingira

5.-(1) Halmashauri imetenga kila siku ya Jumatano ya kila wiki na Jumamosi ya wiki ya mwisho ya kila mwezi kuwa ni siku za wananchi kushiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika maeneo ya Halmashauri.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha kwamba anashiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika siku maalum zilizopangwa na Halmashauri na mwananchi atakayekataa kushiriki katika shughuli za kufanya usafi atakuwa ametenda kosa.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au kiwanja au eneo lolote ambalo halijaendelezwa kufanya usafi katika eneo hilo mara kwa mara.

Mimea Mirefu mjini

6. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kupanda au kuotesha mazao au mimea mirefu katika maeneo ya mjini pamoja na maeneo mengine yaliyozuiliwa na Halmashauri.

Usafi wa mifereji ya maji ya mvua.

7. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba kuondoa uchafu kama vile mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mfereji wa maji ya mvua unaozunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mfereji huo unakuwa msafi, na imara siku zote.

Kusakafia mbele ya jingo

8. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba kuweka sakafu ngumu sehemu ya waenda kwa miguu "pavement" mbele ya nyumba au biashara yake kwa kadri atakavyoelekezwa na Halmashauri.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka biashara ya aina yoyote aidha kwa kuuza au kwa maonyesho katika mfereji au katika pavement au pembeni mwa barabara.

Uwekaji taa za nje ya nyumba

9. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba, mpangaji au mfanyabiashara kuweka taa yenye mwanga nje ya jengo analoishi au analolitumia kwa shughuli yoyote na atatakiwa kuiwasha wakati wa usiku.

Kupaka rangi majengo

10. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha kwamba anapaka rangi nyumba

yake au duka lake ndani na nje kila itakapochakaa.

Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia ya mbu.

11. Itakuwa ni wajibu wa mmiliki wa nyumba kuhakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.

Biashara ya matunda

12. (1)Itakuwa ni wajibu wa kila Mfanyabiashara wa matunda, mbogamboga kuhakikisha kuwa ana chombo maalum cha kuhifadhia maganda au mabaki ya matunda na mbogamboga.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kufanya biashara ya matunda, mbogamboga au miwa pembeni mwa barabara au katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Upulizaji dawa

13. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upuliziaji dawa "Fumigation" au biashara ya kuuwa wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila kuwa na cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na awe na leseni hai kutoka Halmashauri.

Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo

Kuegesha magari mabovu

14. (1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

(2)Ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha magari mabovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi, barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo.

## SEHEMU YA III
## UIMARISHAJI WA AFYA

Usalama wa maji ya kunywa.

15. Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama kwa kuyachemsha au kuweka dawa ya kutibu maji bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji.

Utengenezaji, na uuzaji vyakula.

16. (1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza, kuchoma, kupima, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote

mahali popote mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za afya na amepata kibali kutoka Halmashauri.

Uuzaji vyakula vilivyopi-kwa.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa kuhakikisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi ,aluminiam na kuwekwa kioo kuzuia nzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya kwa binadamu.

Usalama wa vyakula.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini, vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza.

Uzuiaji wa shughuli mbalimbali wakati wa Magonjwa ya mlipuko

17. (1) Afisa Mwidhiniwa atamshauri Mkuu wa Wilaya kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi, au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

Ukamataji wa vyombo vilivyotu-mika kuhifadhia chakula.

(2) Vyakula, vyombo na vifaa vingine vyovyote vitakavyokamatwa baada ya kutolewa amri ya kuzuia kufanyika kwa shughuli hiyo, ambavyo vitakuwa vimetumika kutunzia, kubebea, kuhifadhia na kusafirishia vitaharibiwa na Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea wakati wa utekelezaji wa amri hiyo.

(3) Mtu yeyote atakayekataa kutii amri iliyotolewa atakuwa ametenda kosa.

Maduka ya nyama

18. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama (Bucha) kuhakikisha kwamba duka lake;

(a) ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa tarazo nyeupe hadi urefu wa futi 6 kutoka usawa wa sakafu,

(b) lina maji safi, magogo na misumeno ya kukatia nyama;

(c) lina kabati ya vioo na jokofu la kuhifadhia nyama; sehemu za mizani;

(d) kuna pipa la kuhifadhia taka taka;.

(e) muuzaji ana vazi jeupe pamoja na Apron nyeupe;

(f) muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita

Kuchinja na kuuza nyama mahali pasiporuhusiwa.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja, au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyokuwa machinjio au maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.

(3) Itakuwa ni marufuku kuuza nyama isiyokaguliwa na Afisa Mwidhiniwa

Ufugaji mjini

19. (1)Ufugaji unaoruhusiwa ni wa ndani (zero grazing) kwenye zizi na kwa kuzingatia idadi ya mifugo inayoruhusiwa au katika maeneo yaliyotengwa kama malisho ya mifugo.

Usafi wa zizi

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuachwa kuzurura hovyo mitaani, barabarani au kuchungwa kwenye eneo lolote lisiloruhusiwa.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mfugaji kuhakikisha kwamba sehemu anayotumia kufugia;

(a) inakuwa katika hali ya usafi wakati wote;

(b) anakusanya uchafu wowote utokanao na wanyama kama vile kinyesi, manyoya na nyasi au mabaki ya vyakula na kwenda kutupwa kwenye dampo au kupelekwa shambani kama mbolea.

Uendeshaji wa biashara ya Hoteli na Hosteli.

20. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba za kulala wageni na hosteli au nyumba za biashara kuhakisha anapata kibali kutoka Halmashauri kabla hajaanza biashara,

(2)

Endapo mmiliki hajakidhi masharti ya kiafya Halmashauri inaweza kuzuia kibali cha kuendesha biashara ya hoteli au hosteli mpaka hapo mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti ya kiafya yaliyotolewa na Halmashauri.

Mahitaji Ya nyumba ya wageni na Hosteli

(3) Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, mgahawa, Hoteli na Hosteli kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa mahitaji yafuatayo yamezingatiwa;-

(a) mwanga na hewa ya kutosha;

(b) nafasi na vifaa (samani ) za kutosha;

(c) uimara wa jengo;

(d) mfumo wa uondoshaji wa maji taka, miminika na taka ngumu;

(e) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;

(f) utoshelezaji wa vyoo na mabafu kwa jinsia zote;

(g) vifaa vya zima moto.

(h) tanki la kuhifadhia maji safi; na

(i) vyoo na bafu vimesakafiwa kwa vigae au marumaru na kuta zake zimewekwa vigae kiasi cha futi sita toka usawa wa sakafu.

Upimaji wa afya

21. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mhudumu wa hoteli, mgahawa, baa, bucha sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari au mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza kupima afya kila baada ya miezi sita na watalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha shilingi elfu Kumi na Nane (Tsh.18, 000/=) kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.

(2) Mmiliki yeyote atakayeruhusu mhudumu yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini(50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi 12 jela au vyote kwa pamoja.

Uwezo wa kukagua. Kufungwa kwa jengo la biashara lisilokidhi masharti ya afya.

22. (1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wowote wakati wa

(2)saa za kazi kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi,na endapo atalazimika kufanya kazi nje ya muda wa kazi kibali maalum kitatolewa na Mkurugenzi.

Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kubomoa au kuzuia watu kuishi katika jengo ambalo linahatarisha maisha ya watu na viumbe hai.

(3) Afisa Mwidhinwa atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya chini ya Sheria Ndogo hizi

Ada ya ukaguzi wa afya.

23. (1) Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya ambayo italipwa kwa mwaka kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara.

Viwango vya ada.

(2) Viwango vya ada ya ukaguzi wa afya vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kulipa ada

24. (3) Ada ya ukaguzi wa afya italipwa kila mwanzo wa mwaka wa fedha wa

(4) Serikali, yaani mwezi Julai au wakati mwomba anapokuja kuomba leseni ya biashara.

Kufungua muziki kwa sauti kubwa

Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ada ya ukaguzi atawajibika kulipa kiwango hicho pamoja na adhabu ya asilimia hamsini ya kiwango anachodaiwa.

Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufungulia muziki kwa sauti ambayo itasababisha kelele na kuwa kero kwa wakazi wengine.

Itakuwa ni wajibu kwa kila mmiliki wa kumbi za starehe kuweka vidhibiti sauti (sound proof) kwenye ukumbi wake.

.

## SEHEMU YA III

## UTUPAJI TAKA

Wajibu wa Halma-shauri

25. (1) Halmashauri itatenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka (dampo) na kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji au ghuba hadi kwenye dampo.

(2) Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa Vikundi Jamii (CBOs) na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Wajibu wa kuwa na pipa la taka.

26. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha kuwa ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhia taka ngumu .

Kutupa taka katika sehemu maalum

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba anatupa uchafu, taka, maganda ya matunda, mabaki ya vocha za simu katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalum yaliyotengwa.

Kibali cha kuteketeza taka ngumu

Itakuwa ni wajibu wa kampuni au taasisi inayohitaji kuteketeza taka kuomba kibali na usimamizi wa kuteketeza taka hizo na kulipia ada ya kibali ambayo ni shilingi laki mbili za kitanzania.

Marufuku kutupa taka ovyo

(4) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa taka au uchafu wowote au kuacha kuwepo takataka au uchafu kwenye nyumba, uchochoroni, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara na maeneo ya nyumba au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo.

Uhifadhi maji taka

27. (1) Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.

Kutiririsha maji taka

(2) Ni marufuku kutitirisha au kuelekeza maji, kutoka vyooni, bafuni, karoni, baada ya kufua au kuosha vyombo kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, meneo ya wazi, mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka.

Usajili na malipo ya Biashara ya kunyonya maji taka

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mtoa huduma ya kunyonya maji taka kujisajili kwenye Halmashauri ya Manispaa.

(4) Kila mtoa huduma ya kunyonya maji taka atawajibika kulipia gharama za matumizi ya miundombinu ya maji taka kiasi cha shilingi laki mbili kwa Mwaka.

Taka za viwanda

28. (1) Itakuwa ni marufuku kwa kiwanda chochote kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya na kusababisha kero kwa wakazi wa eneo la Halmashauri.

Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha kiwanda chochote kinachotoa maji taka bila kuwa na mitambo ya kusafishia maji taka hayo ambayo imeidhinishwa na Halmashauri.

Ni marufuku mtu yeyote kuruhusu maji taka kutoka kiwandani au eneo lolote linalofanya utengenezaji kuingiza au kuelekeza katika vyanzo vya maji safi, ardhini, maeneo ya wazi, uchochoroni, mitaro iliyowazi kabla ya kuyasafisha kwa kiwango kinachokubalika na Halmashauri

(4) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha kuwa taka zinazotoka kiwandani kama vile vumbi, maganda, moshi haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe wengine hai.

Uendeshaji wa viwanda

(5) Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengi katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

Ada ya uzoaji taka

29. (1) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kutoka kwa kila kaya au mwenye jengo la biashara kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada ya uzoaji taka italipwa kwa miezi sita au mwaka husika na italipwa kwa Afisa mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kwa malipo yatakayolipwa na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.

(3) Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka , Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Uteuzi wa wakala

30. Halmashauri inaweza kuteua kampuni, kikundi, kikundi cha jamii au Mtu binafsi kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi.

## SEHEMU YA IV

## UJENZI NA MATUMIZI YA VYOO

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

31. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi, imara na madhubuti kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote.

Umbali wa kujenga choo

(2) Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini (60) kutoka kisima au chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya Nyumbani.

Vyoo vya umma

32. (1) Halmashauri inaweza kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au Taasisi kujenga vyoo vya Umma (Public toilet) katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo.

(2) Vyoo hivyo vitamilikiwa na Halmashauri au kwa ubia na wajenzi na vitakuwa ni vya kulipia kama itakavyokuwa imeelekezwa na Halmashauri katika mkataba wake na mawalaka watakaopewa kusimamia vyoo hivyo.

Vyoo vya Muda katika mikusa-nyiko

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu, kikundi, Taasisi yeyote kujenga vyoo vya muda kwa matumizi ya muda huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri.Ikiwa mtu, kikundi au taasisi inalengo la kukutanisha watu kwa madhumuni ya kufanya sherehe, au shughuli yeyote katika eneo ambalo halina vyoo vya kudumu itajenga kwa matumizi hayo na baada ya matumizi vyoo hivyo vitaondolewa.

Vyoo katika majengo ya biashara

(4) Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo viwili hizi kwa ajili ya matumizi ya jinsia za kike na vyoo viwili kwa ajili ya jinsia ya kiume.

Ilani ya kujenga choo

33. (1) Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani ya siku thelathini kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo ikiwa ni pamoja na kumuamuru muhusika kujenga choo kama ambavyo katika Jedwali la tano la Sheria Ndogo hizi.

Kufungwa kwa jengo

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara hadi hapo hali hiyo itakapokuwa imerekebishwa.

Ilani ya Kuondoa kero

34. (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ya siku saba (7) kwa

mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo kama ambavyo inavyoanishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

Mkurug-enzi kuteua mkaguzi

35. (1) Mkurugenzi anaweza kumteua mtu yeyote kuwa mkaguzi kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa usafi katika eneo la Halmashauri.

Uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo

(2) Mkaguzi atakuwa na uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo kwa mtu yeyote atakayekutwa amechafua mazingira kwa kutupa takataka mahali popote pasiporuhusiwa.

(3) Faini itakayotozwa na mkaguzi haitazidi shilingi elfu hamsini.

Makosa

36.Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo;

(a) atamzuia au kujaribu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi; au

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Muidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi,

(c) atamwaga takataka katika mtaa, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni, au mahali popote hadharani au katika eneo lolote la wazi bila idhini ya Halmashauri;

(d) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;

(e) atatirirsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;

(f) ataosha magari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;

(g) atauza vyakula vilivyopikwa barabarani au nje ya majengo mengine;

(h) atafanya matengenezo ya magari, pikipiki na

mitambo, kuendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(i) ataanzisha au kufungua karakana katika majengo au majumba au maeneo ya makazi;

(j) ataenda haja ndogo au kubwa hovyo barabarani, uchochoroni, upenuni au mahali popote ambapo siyo chooni.

(k) atashindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;

(l) atapiga muziki kwa sauti kubwa kwenye maeneo ya makazi bila kuwa na kibali cha Halmashauri.

Adhabu

37. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia kama hakuna adhabu maalumu iliyoainishwa katika kifungu kilichokiukwa atatozwa faini isiyopungua shilingi Elfu Hamsini au kifungo kisichopungua miezi 12 jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA

Limetungwa chini ya kifungu cha 29(1)

Ada ya Uzoaji taka.

| Na. | Eneo. | Kiwango cha ada kwa mwaka |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za kuishi au makazi kwa kaya | 24,000/= |
| 2. | Maduka ya Rejareja, Baa, Grosari, wachoma chips , Kuku, nyamachoma, Saluni, Baba/Mamalishe, Sonara, Mafundi nguo, wachoraji, studio, Waosha magari, Maduka ya kuuza dawa za binadamu, maduka ya kuuza dawa za kilimo na mifugo, Klabu za muziki za usiku, vibanda vya wakala wa mabasi ya mikoani, Masoko kwa chumba, Wauza bidhaa katika magari. | 60,000/= |
| 3. | Mgahawa | 84,000/= |
| 4. | Nyumba za kulala wageni, Wauza mbao au karakana za kuranda mbao, Gereji, Duka la jumla, Vituo vya mafuta, | 120,000/= |

*GN. NO. 159 (Contd)*

| | | |
|---|---|---|
| | Hotel, Godown, Supermarket, Hardware, Hostel, Shule za msingi na sekondari, Vyuo, Sehemu za maonyesho ya biashara,vituo vya kutolea huduma za afya. | |
| 5. | Magenge,Wauza matunda mtaani, | 24,000/= |
| 6. | Ofisi , Taasisi, Kampuni, viwanda vikubwa,Taasisi za fedha, | 300,000/= |

JEDWALI LA PILI
Limetungwa chini ya kifungu cha 23(2)

Ada ya ukaguzi wa Afya

| Na. | Aina ya biashara | Ada kwa mwaka |
|---|---|---|
| 1. | Baa na maduka ya vinywaji (Groceries), Migahawa, mama na baba lishe, maduka ya kuuza nyama ( bucha) | 20,000/= |
| 2. | Nyumba za wageni (Guest House) na Hoteli, kumbi za starehe, mikutano, Hosteli, Viwanda, | 50,000/= |
| 3. | Majengo mengine ya biashara | 10,000/= |

JEDWALI LA TATU

Limetungwa chini ya kifungu cha 21(1)

Ada ya upimaji wa Afya

| Aina ya biashara | Ada kwa miezi sita. |
|---|---|
| Kila mhudumu wa nyumba ya kulala wageni, Hoteli, Mgahawa, cafe, maduka ya nyama (bucha), wauza maziwa, viwanda, maduka ya vyakula, Muuza vyakula vilivyopikwa au kukaangwa anawajibika kujisajili kwa Halmashauri ili kubainisha usalama wa Afya yake kabla ya kutoa huduma kwa wateja kama inavyoelekezwa na sheria ya Afya ya Jamii namba 1 ya Mwaka 2009. Kila mhudumu atapimwa Afya yake kila baada ya miezi sita.(6) | 18,000/= kila anapopimwa |

JEDWALI LA NNE

Limetungwa chini ya kifungu cha 34 (1)

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA

ILANI YA KUONDOA KERO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Manispaa ya Singida, 2018.

SEHEMU 'A'
Ndugu…………………............... wa Mtaa/ Kijiji……………Kata ya …………………Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe …… mwezi ……….. mwaka …. Katika nyumba yako ya Biashara / kuishi / kutolea Huduma / kiwanja * iliyopo eneo la……………………………………………kumekutwa machukizo /kero / uchafu *; kama ifuatavyo;

1) ………………………………………………………………………………..
2) ………………………………………………………………………………..
3) ………………………………………………………………………………..
4) ………………………………………………………………………………..

SEHEMU 'B'
Kwa ilani hii unaamriwa kurekebisha / kuondoa /kusafisha* kwa;

1. ………………………………………………………………………………..
2. ……………………………………………………………………………….
3. ………………………………………………………………………………..
4. ………………………………………………………………………………..

SEHEMU 'C'
Unapewa muda wa siku saba (7) tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza yote yaliyoelezwa katika sehemu 'B' ya Ilani hii, kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kulazimika kukupa taarifa nyingine.

…………………………………..
AFISA MWIDHINIWA

| IMETOLEWA NA; | IMEPOKELEWA NA; |
|---|---|
| Jina;………………………. | Jina;…………………………………. |
| Saini……………………… | saini………………………………..... |
| Wadhifa…………………... | wadhifa…………………………….. |
| Tarehe…………………….. | Tarehe……………………………... |

*Futa lisilohusika

JEDWALI LA TANO

*Limetungwa chini ya kifungu cha 33(1)*

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA

ILANI YA KUJENGA CHOO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Singida, 2017.

SEHEMU ‘A’
Ndugu…………………...............wa Mtaa / Kijiji……………Kata ya…………………Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe……mwezi………..mwaka…. Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma*/ Namba………… iliyopo eneo la ………………katika Kitongoji/Mtaa*……….Kijiji cha…………… Kata ya ………….
Imekuwa haina choo/ choo kimejaa / kimeharibika* hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo;

(1) ………………………………………………………………………………
(2) ………………………………………………………………………………
(3) ………………………………………………………………………………
(4) ………………………………………………………………………………

SEHEMU ‘B’
Unapewa muda wa siku thelathini (30) tu tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza maelekezo na maagizo yote yaliyoelezwa katika sehemu ‘A’ ya Ilani hii,

SEHEMU ‘C’
Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe……………….endepo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itakuchukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine zaidi.

………………………………..
AFISA MWIDHINIWA

| IMETOLEWA NA; | IMEPOKELEWA NA; |
|---|---|
| Jina;………………………. | Jina;…………………………………. |
| Saini……………………… | saini……………………………….... |
| Wadhifa…………………... | wadhifa…………………………….. |
| Tarehe…………………….. | Tarehe……………………………... |

*Futa lisilotakiwa.

HATI YA KUFIFIRISHA KOSA

Mimi…………………………………….. Nakiri mbele ya ………….……. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya SINGIDA /Afisa mwidhiniwa kwa niaba ya Mkurugenzi kwamba mnamo Tarehe……… ya mwezi wa …………………. Mwaka ………. nilikutwa na kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha ……………….. Cha Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Singida za mwaka 2017, Nipo tayari kulipa kiasi cha faini ninachodaiwa kama kifungu cha 37 kinavyoeleza.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe …………………………….. Sahihi…………………………

MBELE YA

Sahihi: ……………………………………………………………

Jina: ……………………………………………………………….

Cheo: ……………………………………………………………..

Tarehe: ……………………………………………………………

*GN. NO. 159 (Contd)*

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida imewekwa katika Sheria Ndogo hizi kufutia Azimio la Baraza la Halmashauri lililoketi tarehe 15 Agosti 2017 katika ukumbi wa Halmashauri na Nembo hiyo iliwekwa mbele ya

BRAVO KIZITO LYAPEMBILE
*Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida*

GWAE CHIMA MBUA
*Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida*

NAKUBALI

Dodoma
12 Februari, 2019

SELEMANI S. JAFO (MB)
*Waziri wa Nchi-or- Tamisemi*